**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI**
**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO CHA KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 CHA TAREHE 23/02/2024**

## MAHUDHURIO

### A: WAJUMBE

| S/N | JINA | CHEO | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe Pancras Maliyatabu | -Diwani Kata ya Mtenga | -Mwenyekiti |
| 2. | William Mwakalambile | -Mkurugenzi Mtendaji(W) | -Katibu |
| 3. | Mhe: Stephen Kayogolo | -Diwani kata ya Isale | -Mjumbe |
| 4. | Mhe: Privatus Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 5. | Mhe: Francis Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 6. | Mhe: Kudra Ahamad | -Diwani Kata ya Kipundu | -Mjumbe |
| 7. | Mhe: Kakuli Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 8. | Mhe: Vitalis Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 9. | Mhe: Mpemba Evarist | -Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 10. | Mhe George Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 11. | Mhe: Loswiata Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 12. | Mhe: Emiliana Kauzeni | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |
| 13. | Mhe: Aida Khenani | -Mbunge Jimbo la Nkasi kaskazini | -Mjumbe |
| 14. | Mhe Vicent Mbogo | -Mbunge Jimbo la Nkasi Kusini | -Mjumbe |

### B WATAALAM

| Na | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Ndg William Mwakalambile | Mkurugenzi Mtendaji (W) |
| 2. | Ndg Immakulata Kushoka | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 3. | Ndg Valeriana Mwapasi | Afisa Mali asili na Uhifadhi Mazingira(W) |
| 4. | Ndg Augustine Bayo | Afisa Elimu Msingi(W) |
| 5. | Ndg Dafrosa Mkenda | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 6. | Ndg Justina Mwita | Afisa Ugavi na Manunuzi(W) |
| 7. | Ndg Mayuma Nzilantuzu | Afisa Usafi na Udhibiti Taka Ngumu(W) |
| 8. | Ndg Emmanuel Gamasa | Kaimu Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji(W) |
| 9. | Ndg John Tlatlaa | Afisa Mifugo na Uvuvi(W) |
| 10. | Ndg Charles Kisanga | Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere |
| 11. | Ndg Erick Kilimo | Kaimu Mweka Hazina(W) |
| 12. | Ndg Victor Makoba | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 13. | Ndg Richard Katyega | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu |
| 14. | Ndg Hussein Membe | Kaimu Mthibiti Ubora wa Shule (W) |

| | | |
|---|---|---|
| 15. Ndg Steward | Vidoga | Kaimu Afisa Mipango na Uratibu(W) |
| 16. Ndg William | Mbinile | Kaimu Mratibu TASAF |
| 17. Ndg Abass | Kiroge | Kaimu Mkaguzi wa Ndani(W) |
| 18. Ndg Barnabas | Mhalila | Kaimu Afisa Biashara, Viwanda na Uwekezaji(W) |
| 19. Ndg Josepha | Joseph | Kaimu Mganga Mkuu(W) |
| 20. Ndg Charles | Claudio | Kaimu Afisa Mawasiliano |
| 21. Ndg John | Ntulo | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 22. Eng Gido | Monji | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi |
| 23. Ndg Nicodemus | Hillu | Kaimu Afisa Ardhi |
| 24. Ndg Emanuel | Hankungwe | Kaimu Mwanasheria wa Halmashaur |

**B SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg Patrick | Kipesha | Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 2. Ndg John | Mnungwasa | Mhudumu wa Ofisi |

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/01/02/2024**
**KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5.15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria na kusisitiza wajumbe kuchangia mawazo kwa kadri ya agenda zilivyoandaliwa na kuwasilishwa mbele yao kwa maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/02/02/2024**
**KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/03/02/2024**
**KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe waliupitia muhtasari wa kikao kilichopita ukurasa kwa ukurasa na kufanya marekebisho yaliyojitokeza kisha walikubali muhtasari utiwe saini kama kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/04/02/2024**
**YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA**

- **Maafisa uvuvi walioko mwambao mwa ziwa Tanganyika wabadilishwe ili kuboresha ukusanyaji wa mapato katika chanzo kitokanacho na mazao ya uvuvi.** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa kwa hatua ya haraka kikao na maafisa uvuvi kimefanyika tarehe 3/01/2024 na kuweka mikakati ya ukusanyaji wa mapato na waliagizwa kutoa taarifa ya utekelezaji kila Mwezi.Aidha wajumbe walitoa ushauri ufuatao.
    - Ni vyema Menejimenti itoe makadirio ya Makusanyo kwa kila Afisa uvuvi kwa Mwezi badala ya kuwahamisha,wajumbe waliunga mkono hoja.

- **Ufuatiliaji ufanyike juu ya adhabu za fedha wanazotozwa Wananchi katika zahanati na vituo vya afya ili kujua kama fedha hizo zinaingizwa katika mfumo.** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa agizo limetekelezwa ufuatiliaji umefanyika katika zahanati na vituo vya afya hakuna kituo kilichobainika kutoza adhabu za fedha kwa wagonjwa hasa mama wajawazito. Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza ufuatiliaji ufanyike suala hili lipo
- Wataalam wa Halmashauri na Makamu Mwenyekiti wafike bandari ya Kigoma kufuatilia ushuru wa mizigo ambayo inasafirishwa kupitia bandari ya Kabwe kutokana na ushuru huo kutolipwa kwa muda mrefu. Katika utekelezaji ilielezwa kuwa ilielezwa kuwa Wataalam hao walifika bandari ya Kigoma tarehe 17/12/2023 kufuatilia takwimu ya bandari ya kabwe na kipili kwa miezi sita (6) na wameahidi kulipa. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;
- Mipaka ya kudumu iwekwe katika Hifadhi ya msiti Mfili na taarifa ya ukubwa wa msitu huo iwasilishwe katika kikao kijacho. Katika utekelezaji ilielezwa kuwa agizo limetekelezwa mipaka ya kudumu ilishawekwa kinachotakiwa kwa sasa ni kufyeka mipaka hiyo yenye upana wa mita 6 hadi 10 ili uonekane kwa Wananchi kwa urahisi kuhusu ukubwa wa eneo la msitu ni ekari 3627.8. Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza Msitu huo ulindwe.

- Taka taka zilizolundikana katika maghuba yaliyoko mjini Namanyere ziondolewe ili kuepusha mlipuko wa magonjwa unaoweza kutokea na kuondoa kero kwa wananchi waliopo karibu na maghuba hayo. Katika utekelezaji ilielezwa kuwa agizo limetekelezwa takataka zimezolewa. Wajumbe walipokea taarifa na kupongeza kwa kazi nzuri na kuomba kazi hii iweze kuendelea na kutoruhusu uchafu kurundikana tena katika maeneo hayo.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/05/02/2024**

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA 2023**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa Mwezi Disemba 2023. Aliwaeleza wajumbe kuwa Katika kipindi cha mwezi Disemba 2023 Halmashauri imekusanya mapato ya ndani kutoka vyanzo vyake Jumla ya Tshs. 134,070,962 Hivyo kufanya kiasi kilichokusanywa kuanzia Julai 2023 hadi Disemba 2023 kuwa Jumla ya Tshs 1,355,606,011 sawa na asilimia 43 ya bajeti ya mwaka 2023/24 ya Tshs 3,133,755,000.00

Aidha Halmashauri kwa mwezi Disemba 2023 ilipokea fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kama ifuatavyo: -Mishahara Tshs 21,082,510,000.00, Matumizi mengineyo Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs 1,465,102,000.00, Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeeo Halmashauri ilipokea kiasi cha Tshs 11,994,167,200.00. Hivyo kuanzia mwezi julai 2023 hadi Disemba 2023 Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs 5,958,900,650,000.00 sawa na asilimia 45 ya makisio ya mwaka

Katika kipindi cha mwezi Disemba 2023 Halmashauri ilitumia kiasi cha Tshs 279,051,324 kutoka mapato ya ndani. Hivyo kufanya fedha zilizotumika Mwezi Julai 2023 hadi Disemba 2023 kuwa Tshs 2,704,408,871.00 sawa na asilimia 23 ya bajeti ya mwaka; Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo.

-Mjumbe alitaka kujua deni la bima ya afya kwa waheshimiwa madiwani kama limeshalipwa

-Mjumbe mwingine alishauri kamati ya fedha, Utawala na Mipango ishirikishwe ipasavyo katika fedha za miradi ya maendeleo ili kuweza kujua kinachoendelea ili waweze kushauri.

-Mjumbe mwingine aliomba maafisa uvuvi wahamishwe katika vituo vyao na kupelekwa vituo vingine kwani mapato mengi yanapotea kwa kupitia wao.

-Mjumbe mwingine alishauri fedha za miradi ya maendeleo zinapoingia zitumike kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

-Wajumbe walishauri vyanzo vipya vya mapato viibuliwe ili kupandisha mapato ya Halmashauri

-Mjumbe mwingine alishauri matumizi ya fedha zinazokusanywa zitumike vizuri ili kuweza kuleta maendeleo kwa Wananchi

-Mjumbe mwingine alishauri mapato ya papo kwa papo katika zahanati na vituo vya afya zikusanywe na kuingizwa katika mfumo. Baada ya majadiliano ya kina Mweka hazina kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) alipokea ushauri na kutolea ufafanuzi wa hoja kama ifuatavyo;

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/07/02/2024**
**KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA KWA ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

Idara zifuatazo ziliwasilisha taarifa

**I. IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI**

Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Idara kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazokabili Idara kama ifuatavyo; Vibali vya ajira mpya na mbadala kutotolewa kwa wakati, upungufu wa vitendea kazi kama magari, pikipiki na kompyuta, upungufu wa nyumba za Watumishi hasa Watendaji Kata na vijiji pamoja na uhaba wa Watumishi hasa Idara ya Afya, Elimu, Utawala, Sheria, Ugavi na Manunuzi, Ardhi, Kilimo na Mifugo.Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Wajumbe walipokea taarifa na kushauri idara iendelee kuomba vibali vya ajira ili kuweza kukabiliana na upungufu uliopo.

**II. IDARA YA MIPANGO NA URATIBU**

Kaimu Afisa mipango na Uratibu (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazokabili Idara kama ifuatavyo; Fedha za Maendeleo zilizokasimiwa katika bajeti kutofika kwa wakati toka Serikali Kuu, hivyo kupelekea miradi ya Maendeleo kutotekelezwa kwa wakati. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alishauri Idara ya Mipango na Uratibu kutembelea miradi kwa wakati na kutoa ushauri pale panapohitajika. Baada ya hapo Wajumbe waliunga mkono hoja.

**III. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI**

Kaimu Mkaguzi wa Ndani(W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na kitengo kwa robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia aliwasilisha changamoto zinazokabili kitengo kama ifuatavyo; ukosefu wa chombo cha usafiri kwa ajili ya shughuli za ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi mbalimbali ndani ya Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa na kushauri Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kitumie magari yaliyopo kwani magari kwa sasa ni mengi ambayo yatarahisisha kazi zao

**IV. KITENGO CHA SHERIA**

Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri aliwasilisha taarifa ya shughuli zilizofanyika kwa kipidi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia aliainisha changamoto zinazokabili kitengo kuwa ni pamoja na Uelewa mdogo wa mambo ya kisheria katika Jamii, ucheleweshaji wa migogoro ya kisheria kuripotiwa katika kitengo, Kuchelewa kwa maelekezo na miongozo mbalimbali ya kisheria pindi mabadiliko yanapotolewa na Serikali na upungufu wa vitendea kazi. Wajumbe walipokea taarifa na kupongeza kitengo cha Sheria kwa kusimamia kesi mbalimbali. Wajumbe waliunga mkono hoja.

## V. KITENGO CHA TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO

Kaimu Afisa TEHAMA (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa kwa robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia alieleza changamoto kama ifuatavyo; uchakavu mkubwa wa vifaa vya kukusanyia mapato (POS Mashine), Ukosefu wa vitendea kazi na ukosefu wa usafiri wa kufika maeneo mbalimbali ya Wilaya kwenda kutatua changamoto za kimfumo. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alishauri ili kuweza kuongeza mapato katika Halmashauri kila kituo cha kukusanyia mapato kiwe na Mashine ya kukusanyia mapato (Pos Mashine) hivyo kitengo kijitahidi kutengeneza Mashine za kukusanyia mapato zilizo mbovu

## VI. KITENGO CHA UGAVI NA MANUNUZI

Kaimu Afisa Ugavi na Ununuzi (W) aliwasilisha taarifa ya majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa kwa robo ya pili kwa mwaka 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazo kabili kitengo kama, upungufu wa Watumishi na uhaba wa vitendea kazi. Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kitengo kufanya kazi kwa weledi ili miradi mbalimbali iweze kukamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

## VII. TAARIFA YA TASAF

Kaimu Mratibu wa TASAF(W) aliwasilisha taarifa ya kazi mbalimbali zilizotekelezwa na TASAF kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Wajumbe walipokea taarifa na kuunga mkono hoja

### AGENDA NA NKS/DC/FUM/08/12/2023
### KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI KWA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO YA TAREHE 31/01/2024 MPAKA TAREHE 01/02/2024

Kaimu Afisa Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa ya ukaguzi wa miradi iliyofanywa na Kamati ya Fedha, Utawala na mipango kuanzia tarehe 31/01/2024 mpaka tarehe 01/02/2024. Aliwaeleza wajumbe kuwa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango imefanya ziara ya ukaguzi wa miradi kuanzia tarehe 31/01/2024 mpaka tarehe 01/02/2024 ilipitia miradi 10 inayotekelezwa katika Wilaya ya Nkasi na kila sehemu waliacha maagizo na maelekezo. Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kuwa maagizo mbalimbali katika miradi hiyo yafanyiwe kazi

### AGENDA NA NKS/DC/FUM/09/12/2023
### MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Katika kikao hiki mengineyo yaliyojitokeza ni pamoja na

### AGENDA NA NKS/DC/CMT/10/12/2023
### KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 10.07 jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA**

……………………………… ……………………………

WILLIAM, A MWAKALAMBILE PANCRAS, C MALIYATABU

**KATIBU** **MWENYEKITI**

TAREHE 22 / 03 / 2024

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NKASI

THE CHAIRMAN
NKASI DISTRICT COUNCIL